

Kinachoendelea Baada ya FBME Kuwasilisha Maoni FinCEN

14 Octoba, 2014

Tarehe 22 Septemba, Benki ya FBME iliwasilisha maoni yake ya umma kwa Idara ya Hazina ya Marekani FinCEN ambapo ilijibu kwa ufasaha masuala yote yalioainishwa na FinCEN kwenye Azimio la Matokeo na Azimio la Mapendekezo ya Maamuzi iliyotolewa Tarehe 15 Julai, 2014 na kutangazwa kwenye daftari la shirikisho tarehe 22 Julai, 2014.

FinCEN imethibitisha kuwa inayapitia maoni ya Benki na kuyapa zingatiao linalostahili kwa mujibu wa sheria na kanuni. za FinCEN. Benki ya FBME itaendelea kujishirikisha katika mijadala zaidi na FinCEN.

FBME imeiweka ripoti yake inayopatikana kwenye tovuti ya www.fbmeltd.com iliyoijibu ndani ya kipindi cha siku 60 kinachoruhusiwa kuwasilisha maoni.

Wasilisho la Benki ya FBME, liliyoandaliwa na kampuni ya sheria ya kimataifa ya Hogan Lovells kwa msaada wa wahasibu wa uchunguzi wa Ernst & Young (EY), lilionyesha ari ya kujitolea kufuata taratibu za kutoitumia Benki kwa madhumuni haramu, na kutoa ushirikiano usio na masharti kwa kufanya kazi na FinCEN na Mamlaka nyingine yoyote ya kuzuia uhalifu wa kifedha wakati wowote na popote kwa jinsi itakavyowezekana.

Kulingana na mapitio ya uchunguzi uluofanywa na Hogan Lovells na EY, benki ya FBME, kwa heshima imeiomba FinCEN kwenye wasilisho hilo kwamba Ilani za NPRM ziondolewe. Huu ndio msimamo wa Benki.

Benki ya FBME ilitoa msimamo wake rasmi katika majibu yake:

"Benki ya FBME itaendelea kushirikiana na Serikali ya Marekani pamoja na serikali ya Cyprus na Tanzania, katika mapambano dhidi ya fedha chafu na kusaidia kuwafadhili magaidi. FBME imewekeza rasilimali za kutosha kwa kuendeleza na kuimarisha mifumo yake katika kupambana na fedha chafu ("AML") na mpango wa Vikwazo ("Compliance Program" au "Program") ili kuendana na viwango vya Ulaya, Cyprus na Tanzania. "

EY ilifanya uchunguzi wa kina na huru wa sera za Benki ya FBME na taratibu za uendeshaji hasa kuhusiana na taratibu za kupambana na fedha chafu. Kama EY ilivyogundua kwenye tathmini yake:

Sera za Benki ya FBME za AML (kupambana na pesa chafu) zinarandana na mahitaji ya Ulaya (EU) na Benki Kuu ya Cyprus

Maoni yanaeleza hatua ambazo Benki ya FBME imechukua kuimarisha programu yake ya kupambana na fedha chafu katika miaka ya karibuni, na kwamba imetekeleza mfumo kulingana na mahitaji mamlaka husika.

Benki inaahidi kuendelea kuongeza programu yake ya kupambana na fedha chafu hadi kuiridhisha FinCEN.

Katika hatua nyingine, Benki ya FBME inakaribisha nafasi ya kushirikiana zaidi na FinCEN, hasa kuhusiana na tathmini ya Mpango wa Kuzuia Fedha Chafu ili kuboresha mifumo ya FBME ili kwamba FBME na wateja wake waweze kuanza tena shughuli halali za biashara zao haraka iwezekanavyo.

Mwanzo Wake: Kuhusu FBME Bank

FBME ni Benki ya Biashara inayoongoza ikiwa na rekodi nzuri ya kuwahudumia wateja wake wa kimataifa. Mafanikio ya Benki yamejengwa juu ya misingi ya kihafidhina inayolenga zaidi katika kutoa huduma ya daraja la kwanza na faida imara.

Asili ya Benki inakwenda nyuma hadi mwaka 1952, wakati Benki ya Shirikisho la Lebanon SAL (FBL) ilipoanzishwa na Bwana Michel Saab. Kufuatia kuzuka kwa vita katika Lebanon, Benki ya Federal bank of Middle East iliundwa nchini Cyprus mwaka 1982 Benki ilibadili jina lake na kuwa FBME Limited mwaka 2005. FBME Bank Limited na Federal Bank of Lebanon SAL leo hii ni makampuni tofauti ingawaje zinamilikiwa na wamiliki sawa.

Mwaka 1982 FBME Bank Limited tawi la Cyprus ilipewa leseni ya Biashara ya Kibenki ya kufanya kazi ndani ya nchi chini ya usimamizi wa Benki Kuu ya Cyprus. Hadi sasa FBME Bank Limited simefanya kazi nchini Cyprus kwa zaidi ya miaka 30.

Awali iliundwa chini ya umiliki kati ya mwanzilishi, Bwana Michel Saab na wanawe. Tangu alipofariki Bwana Michael Saab mwaka 1991, FBME Limited imekuwa ikimilikiwa sawa kati ya Bwana Ayoub-Farid M Saab na Bwana Fadi M Saab.

Kupitia kampuni tanzu na vitengo vyake, mpaka katikati ya Julai mwaka 2014, Benki ya FBME imeajiri wafanyakazi 438 wa Cyprus, Tanzania na Urusi. Kati ya hao raia 200 ni wa Jamhuri ya Cyprus. Wateja wake wanatoka maeneo tofauti kijiografia duniani takriban nchi 50 tofauti.

Mgogoro na Benki Kuu ya Cyprus (CBC)

Kufuatia taarifa ya FinCEN ya Julai 15, wanahisa wa FBME waliialika Benki Kuu ya Cyprus kufuatilia shughuli zake. Mara tu baada ya kutaarifiwa kuhusu Ripoti ya FinCEN, FBME alichukua hatua zote sahihi ndani ya masaa 24 ya kwanza.

Pamoja na hatua hizi za FBME, CBC haraka ilitangaza kuchukua udhibiti wa Benki ya FBME tawi la Cyprus na kuliweka chini ya sheria ya Azimio la Cyprus inayolenga mabenki yenya amana inayolegalega.

Hoja ya CBC kuichukua Benki ni ya kiujanja – Benki ya FBME ilikuwa na bado itaendelea kuwa na amana ya kutosha. Katikati ya mwezi Julai, Benki ilikuwa na uwiano wa ukwasi wa muda mfupi wa asilimia 104. Hata hivyo, CBC iliwawekea wateja vikwazo vya upatikanaji wa fedha zao hata kama benki ingeweza kulipa madai yote ya wateja.

Tarehe 21 Julai, baada ya masaa 24 tu ya udhibiti wa Benki Kuu, CBC ilitoa Amri ya uuzaji wa tawi la FBME katika Jamhuri ya Cyprus na wakati huo huo kuwasilisha taarifa hizi kwa wamiliki wa FBME.

Benki ya FBME kwa upande wake inaichukulia hatua hii kama uvamizi na kwa sasa imefungua kesi kwenye mahakama ya Cyprus kupinga hatua hiyo.

FBME inafungua jalada la maombi ya usuluhishi kwenye mahakama ya kimataifa ya usuluhishi (ICC) huko Paris. Usuluhishi unatengua mkataba wa Lebanon-Cyprus wa kukuza ubadilishanaji na ulinzi wa uwekezaji (sheria na 399).

Wanahisa wa FBME wamewasilisha maombi ya Muda Agosti 14, 2014 kwenye Mahakama ya Wilaya ya Nicosia kuunga mkono kesi ya usuluhishi. Mahakama ya Wilaya ya Nicosia itasikiliza kesi tarehe 21 Oktoba.

CBC na Mamlaka ya Azimio wameahidi kutokufanya makubaliano ya kisheria kuhusu uuzaji wa tawi la Benki mpaka hukumu itakapotolewa juu ya shauri la muda mfupi, ingawaje hawakuondoa dhamira yao ya kuiuza Benki.

FBME anaamini kwamba hatua ya CBC inaiondolea sifa Cyprus kama kituo cha biashara ya benki cha kimataifa. Vitendo vya CBC vimeweka maisha ya wafanyakazi wa FBME kwenye hatari. FBME Bank tayari imelazimika kuwaachisha kazi wafanyakazi 70 kati ya 105 katika Kitengo chake cha huduma za kadi.

Benki ya FBME itaendelea kupigania kile inachoamini kuwa ni uvamizi haramu kwa Benki kutoka Benki Kuu ya Cyprus.